## MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI KITAIFA MKOANI DAR E SALAAM - 1 DESEMBA, 2013

## HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII MH. DK. HUSSEIN MWINYI (MB)

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam

Waheshimiwa Mawaziri,

Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Waheshimiwa Wabunge,

Waheshimiwa Mabalozi

Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania,

Wadau wa Maendeleo katika Mapambano dhidi ya UKIMWI nchini,

Mwenyekiti wa Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI,

Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Viongozi wa Dini,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana

**Mheshimiwa Rais,**

Awali ya yote, nachukua nafasi hii kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Said Mecky Sadick kwa kunialika katika siku hii muhimu ya kutafakari hatua tuliyopiga ndani ya kipindi hiki cha miongo mitatu ya mapambano dhidi ya UKIMWI nchini.

Ninaamini kwamba, kupitia fursa hii adhimu niliyoipata, watu waliokusanyika katika hadhara hii na wengine ambao hawapo hapa, kupitia vyombo vya habari, watafahamu kwa muhtasari, mikakati mbalimbali inayotekelezwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kutokomeza maambukizi mapya ya VVU, vifo vinavyotokana na UKIMWI na unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na UKIMWI ambayo ndio shabaha yetu kama nchi ifikapo mwaka 2015.

**Mheshimiwa Rais,**

Siku kama ya leo mwaka jana (2012) Mkoani Lindi, ulizindua Mpango wa Taifa wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kwa watoto ifikapo mwaka 2015 sambamba na kuzuia vifo vya kina mama vinavyotokana na uzazi. Katika Mpango huu, Serikali imedhamiria kupunguza maambukizi mapya ya VVU kwa watoto kutoka asilimia **26** mwaka 2010 hadi kufikia asilimia **4** ifikapo mwaka 2015. Aidha kwa takwimu za mwaka 2012, maambukizi ya VVU kwa watoto yamepungua hadi kufikia asilimia **15.**

Aidha, ninapenda kukufahamisha kwamba, tayari Wizara yangu imeanza kutekeleza Mpango uliouzindua mwaka jana ambapo hivi sasa, mikoa 9 ya Tanzania Bara imeanza kutekeleza Mpango huu na mingine 16 iliyobaki itafuata kwa awamu. Katika utekelezaji wa Mpango huu, wajawazito na wanawake wanaonyonyesha wenye Virusi vya UKIMWI wanapewa dawa za kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI, dawa ambazo watatumia kwa maisha yao yote.

**Mheshimiwa Rais,**

Hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2012, huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, ilikuwa ikitolewa bila malipo katika vituo **4,914** nchi nzima ambavyo ni sawa na

asilimia **97** ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto.

Aidha, kwa mwaka 2012, kati ya wajawazito **69,937** waliogundulika kuwa na virusi vya UKIMWI, miongoni mwao, **44,799** walipatiwa dawa za ARVs ili kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Hii ni sawa na asilimia **75** ya wajawazito wote waliokuwa na maambukizi ya VVU katika jamii kwa mwaka huo.

**Mheshimiwa Rais,**

Hadi kufikia Desemba 2012, jumla ya vituo vipatavyo **1,660** vilikuwa vinatoa huduma ya utambuzi wa mapema wa hali ya maambukizi kwa watoto wanaozaliwa na kina mama wenye maambukizi ya VVU. Huduma hii imekuwa ikiongezeka ambapo katika kipindi cha mwaka mmoja, kuanzia Julai 2012 hadi Juni mwaka huu (2013), jumla ya watoto **25,240** waliozaliwa na kina mama wenye maambukizi ya VVU walifikiwa na huduma hii ambayo ni sawa na asilimia **80%** ya watoto wote walioandikishwa.

**Mheshimiwa Rais,**

Wizara yangu inaendelea kutekeleza afua ya tohara katika mikoa **12** yenye viwango vya juu vya maambukizi ya VVU na wakati huohuo ina viwango vya chini vya tohara. Mikoa hiyo ni pamoja na Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Mara, Mbeya, Mwanza, Njombe, Rukwa, Shinyanga, Simiyu, na Tabora. Hadi kufikia mwezi Septemba mwaka huu (2013), Jumla ya wanaume **676,225** ambayo ni sawa na asilimia **24** ya lengo lililokusudiwa, walikuwa wametahiriwa katika mikoa hiyo. Wizara yangu inaandaa Mpango wa Utekelezaji wa huduma ya tohara ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

**Mheshimiwa Rais**

Tangu kuanzishwa kwa Mpango wa Damu Salama, kumekuwepo na ongezeko la wachangia damu wa hiari kutoka kiasi cha chupa **5,000** mwaka 2005 hadi kiasi cha chupa **160,445** mwaka 2013. Aidha, upatikanaji wa uhakika wa damu salama, umepunguza hatari ya maambukizi ya maradhi yanayoambukizwa kwa njia ya damu hususani VVU. Kiwango cha VVU toka kwa wachangia damu wa hiari kimeshuka kutoka asilimia **7.0** mwaka 2006 hadi chini ya asilimia **1** mwaka 2013. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuboresha zaidi upatikanaji wa damu salama ili hatimaye, kiwango cha maambukizi ya VVU kwa kuchangia damu nacho kishuke hadi sifuri.

**Mheshimiwa Rais,**

Kitendo ulichokionyesha tarehe 14 Mwezi Julai mwaka 2007, wakati unazindua Kampeni ya Taifa ya Kupima VVU ambapo wewe na mke wako Mama Salma Kikwete mlipima pamoja, ni kitendo cha kizalendo na ni mfano wa kuigwa miongoni mwetu. Ninaamini, siku ile mlipata ushauri nasaha pamoja, mlipima pamoja na kupokea majibu pamoja. Ninatoa rai kwa watanzania wenzangu wenye mahusiano ya kimapenzi na hasa wenzi, kuiga mfano huu, kwani wenzi wanapopima na kupokea majibu pamoja, wanapata faida nyingi ikiwemo fursa ya kupanga mipango ya huduma na tiba kwa pamoja endapo mmojawapo au wote wawili watakuwa na maambukizi ya VVU. Wanapopima pamoja, wenzi pia wanarahisisha ushirikishanaji wa majibu ya VVU miongoni mwao .

**Mheshimiwa Rais**

Wizara yangu inaendelea kutoa huduma na tiba kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Huduma hii ambayo ilianza kutolewa nchini bila malipo mwaka 2004, imewanufaisha watanzania wengi mijini na vijijini,

wakubwa kwa watoto. Hadi kufikia Mwezi Juni mwaka huu (2013), watanzania wapatao **1,209,686** walikuwa wameorodheshwa kwenye huduma za tiba na matunzo ya UKIMWI na miongoni mwao, watu **736,664** walikuwa wameanzishiwa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI ambazo zinapatikana bila malipo katika vituo **1,176** vinavyotoa huduma hiyo nchi nzima.

**Mheshimiwa Rais,**

Mwongozo wa Kitaifa unataka watoto wote wenye umri chini ya miaka miwili wenye maambukizi ya VVU waanzishiwe dawa za ARV. Hata hivyo, baadhi ya watoto wanaoishi na VVU nchini wamekuwa wakikosa huduma hii muhimu kwa mustakabali wa maisha yao. Kati ya watu **1,209,686** walioorodheshwa kwenye huduma za tiba na matunzo ya UKIMWI, kuna watoto **91,283** ambao ni sawa na asilimia **26** tu ambao wameorodheshwa huku miongoni mwao, watoto **60,572** wakiwa wanatumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Ninawaasa, wazazi na walezi wa watoto wanaoishi na VVU, kuwapeleka watoto wao katika huduma za tiba na matunzo, kwani upatikanaji na matumizi sahihi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI unatoa fursa kwa watoto wenye VVU kukua wakiwa na afya njema, kwenda shule, kufikia utu uzima na hata kuanzisha familia zao.

**Mheshimiwa Rais,**

Ili kupanua huduma ya upimaji wa kinga mwili (CD4) kwa watu wanaoishi na VVU, hivi karibuni Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine, imepanua wigo wa upatikanaji wa huduma hiyo kwa kununua na kusambaza mashine za kupima CD4 zipatazo **450** nchi nzima. Mashine hizo ambazo zina uwezo wa kutoa majibu ndani ya muda mfupi zaidi, zimesambazwa katika baadhi ya vituo vya afya na zahanati

nchi nzima hivyo kupelekea zaidi ya asilimia **50** ya kliniki zinazotoa huduma ya tiba na matunzo kutoa huduma ya upimaji wa CD4. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu inakusudia kuongeza mashine zingine zipatazo **105.**

**Mheshimiwa Rais,**

Hivi karibuni tumepokea, kutoka Serikali ya Marekani msaada wa mashine za CD4 zipatazo **21 .** Mashine hizo, zitasambazwa katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Ruvuma na Mbeya. Leo hii tutakuomba umkabidhi mashine moja ya CD4, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Dk. Rajab Mtumwa Rutengwe, kwa niaba ya Wakuu wa Mikoa wengine. Mashine hiyo inawakilisha mashine hizo zitakazogaiwa katika mikoa husika.

**Mheshimiwa Rais,**

Tarehe 27 Machi mwaka huu, wakati unazindua Ripoti ya Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI na Malaria ya mwaka 2011/2012, ulitamka, ninanukuu *"Tumepata mafanikio mengi sana lakini mapambano yenyewe bado kabisa – kwa sababu bado kuna changamoto mbili kubwa – moja ni kuzuia maambukizi mapya na pili kuhakikisha wote ambao wameathirika wanaendelea kupatiwa dawa za kurefusha maisha."* mwisho wa kunukuu. Ninakuahidi kwamba, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tutaongeza kasi ili malengo tuliyojiwekea yatimie.

**Mheshimiwa Rais,**

Kwa kumalizia, napenda kukufahamisha kwamba, mafanikio ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana na UKIMWI yameweza kufikiwa kutokana na juhudi na rasilimali mbalimbali zilizotolewa na Serikali na wadau wake.

Tunawashukuru sana wadau wetu kwa kuelewa nia yetu na kutuunga mkono hadi sasa. Nachukua fursa hii kuwashukuru wadau wafuatao:

- Serikali ya Marekani
- Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria
- Mashirika ya Umoja wa Mataifa
- Serikali ya Japan kupitia Shirika la Msaada la JICA
- Umoja wa Ulaya
- Wadau wa Pamoja wa Mfuko wa Afya
- Na wadau wengine wote

Kwa namna ya pekee, ninatoa rai kwa wadau wetu, ndani na nje ya nchi, waendelee kutuunga mkono katika mapambano dhidi ya UKIMWI hapa nchini ili nasi siku moja tuwe ni jamii inayoishi bila ya maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vinavyotokana na UKIMWI.

***Ahsanteni kwa kunisikiliza***